



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI
MAONESHU YA NANENANE KWA MWAKA 2020**

***Ndugu Wanahabari,** nimewaita leo hapa ili niweze kuzungumza nanyi na umma wa Watanzania wote kuhusu Maonesho ya Nanenane kwa Mwaka 2020.*

Ndugu Wanahabari,

Kama mnavyofahamu, Nchi yetu huadhimisha Sherehe za Wakulima na Maonesho ya Kilimo **NANENANE** kila Mwaka kuanzia **tarehe 01 hadi 08 ya Mwezi Agosti**. Maonesho hayo huambatana na uhamasishaji wa matumizi ya teknolojia bora za kilimo, ufugaji na uvuvi. Pia, maonesho hayo hushirikisha Wadau mbalimbali zikiwemo Wizara, Taasisi za Umma na Binafsi, Wabia wa maendeleo, wakulima na Vyama vya wakulima, wafugaji na wavuvi.

Ndugu Wanahabari,

Napenda kuutarifu umma wa Watanzania kuwa Maonesho ya Nane Nane kwa Mwaka 2020 yatafanyika nchini kuanzia **tarehe 01 hadi 08 Agosti, 2020 ikiwa ni Maonesho ya Ishirini na Nane (28) tangu kuanzishwa kwake mwaka 1993**. Maonesho hayo yatafanyika kwenye Kanda nane (8) za Maonesho ambazo ni Kanda ya Mashariki (**Morogoro**), Kanda ya Kaskazini (**Arusha**), Kanda ya Magharibi (**Tabora**), Kanda ya Kusini (**Lindi**), Kanda ya Kati (**Dodoma**), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (**Mbeya**), Kanda ya Ziwa Mashariki (**Simiyu**) na Kanda ya Ziwa Magharibi

(Mwanza). Kitaifa, Maonesho hayo yatafanyika katika viwanja vya Nyakabindi, Wilaya ya Bariadi Mkoani Simiyu.

Ndugu Wanahabari,

Kupitia Maonesho hayo, Viongozi mbalimbali wa Kitaifa watatembelea viwanja vya Maonesho na kuhamasisha masuala mbalimbali ya kuendeleza sekta za kilimo, mifugo, uvuvi pamoja na Ushirika. Baadhi ya Viongozi wanaotarajiwa kushiriki katika Maonesho hayo ngazi ya Taifa ni Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ndugu Wanahabari,

Lengo la Maonesho ya Nanenane ni kutoa fursa kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na wanaushirika kuona na kujifunza matumizi ya teknolojia bora za kilimo, ufugaji na uvuvi kwa ajili ya kuongeza tija na uzalishaji kwa uhakika wa chakula, kukidhi mahitaji ya viwanda na masoko ya ndani na nje ya nchi.

Ndugu Wanahabari,

Kaulimbiu ya Maonesho ya Mwaka 2020 ni "**Kwa Maendeleo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Chagua Viongozi Bora 2020**". Kwa kuwa Mwaka 2020 ni Mwaka wa Uchaguzi Mkuu, Kaulimbiu hiyo inatoa hamasa kwa wananchi kuchagua viongozi bora watakaokuwa chachu ya kuleta mapinduzi kwa ajili ya maendeleo ya sekta za kilimo ili kuinua ustawi wa maisha ya wakulima, wafugaji na wavuvi.

Ndugu Wanahabari,

Napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa wadau wote wa sekta ya umma na binafsi kukamilisha maandalizi ya kushiriki katika viwanja vyote vya maonesho vilivyopo kwenye Kanda Nane (8) kama nilivyoieleza hapo juu. Aidha, Kamati za Maandalizi ya Nanenane ngazi ya Kanda zinazoongozwa na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa zihakikishe zinakamilisha maandalizi yote muhimu na kuwashirikisha wadau wote.

Ndugu Wana habari,

Katika kuhakikisha Maonesho ya Kilimo yanakuwa na tija, Wizara ya Kilimo iliandaa na kusambaza katika mikoa yote **Mwongozo wa Maonesho na Mashindano ya Kilimo, Mifugo Na Uvuvi. Mwongozo huo, pamoja na mambo mengine unaeleza Utaratibu wa Kusimamia na Kuratibu Maonesho ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ikiwemo majukumu ya kila mdau; Matumizi Endelevu ya Viwanja Vya Maonesho; Mapato na Matumizi kwa ajili ya Maonesho; na Ufuatiliaji na Tathmini.** Hivyo, nisisitize Uongozi wa Mikoa katika Kanda zote uhakikishe kuwa Maonesho ya Nanenane yanafanyika kwa kuzingatia Mwongozo huo. Aidha, kama ilivyoelezwa katika Mwongozo wa Maonesho, ni lazima mikoa ihakikishe viwanja vya Maonesho vinatumika muda wote kabla, wakati na baada ya maonesho kama mashamba darasa na vitovu vya kutoa elimu ya matumizi bora ya teknolojia bora za uzalishaji na masoko.

Ndugu Wanahabari,

Nirudie tena kutoa wito kwa Wizara, Taasisi, Wakala, Mashirika, Sekta Binafsi na wadau mbalimbali kujitokeza kwa wingi kushiriki kushiriki kwenye maonesho ya Mwaka huu. Aidha, ninasisitiza waoneshaji wote kuwa na ubunifu katika kutoa elimu na kuonesha teknolojia zinazokidhi mahitaji ya wazalishaji na walaji wa mazao na bidhaa mbalimbali zinazozalishwa hapa nchini.

Kwa mawasiliano zaidi kwa ajili ya ushiriki katika maonesho ya Nanenane kwa Mwaka 2020, yafanyike kupitia kwa Namba za Simu zifuatazo: **0754 475502 na 0713 429501.**

Ndugu Wanahabari,

Jambo la pili ambalo nilitaka nizungumze nanyi na umma wa Watanzania siku ya leo ni kuhusu msimu wa ununuzi wa kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA).

Ndugu Wanahabari,

Sote tunafahamu kuwa Mkoa wa Songwe ulishika nafasi ya tatu Kitaifa katika uzalishaji wa mazao ya chakula nchini katika msimu wa 2018/19. Kutokana na uzalishaji huo mkubwa wa chakula, Serikali imeona ipo haja ya kuanzisha Kanda ya NFRA katika Mkoa wa Songwe, tofauti na hapo awali ambapo hapa Vwawa palikuwa na Kituo kidogo cha NFRA ambacho kilikuwa chini ya Kanda ya NFRA Makambako.

Ndugu Wanahabari,

Kanda ya NFRA Songwe ilianzishwa rasmi tarehe 01 Julai, 2020 na inatarajiwa kuhudumia Mikoa ya Songwe na Mbeya. Kuanzishwa kwa Kanda hii kumetokana na hali ya uzalishaji mkubwa wa chakula katika Mikoa ya Songwe na Mbeya, pamoja na kujengwa kwa Maghala na Vihenge vya Kisasa ambavyo vitaongeza uwezo wa uhifadhi kutoka tani 17,000 za awali na kufikia tani 37,000.

Ndugu Wanahabari,

Katika Kituo cha Vwawa, zoezi la ununuzi wa mahindi limeanza rasmi tarehe 06 Julai, 2020. Kwa sasa tunaanza na ununuzi wa tani 10,000 na tunanua kwa bei ya 550 kwa kilo. Tutaendelea kuongeza kiasi cha ununuzi kadri tunavyopata fedha kutoka Serikalini. Napenda kuwajulisha kuwa, mtu yeyote anaruhusiwa kuuza mahindi NFRA bila kujali upendeleo wowote ilimradi mahindi hayo yawe na ubora unaotakiwa.

Aksanteni sana kwa kunisikiliza.

Imetolewa na;

Japhet N. Hasunga (Mb.)
WAZIRI WA KILIMO
08 JULAI, 2020